

MBOLEA ZA ASILI

MWANDISHI: Mkulima mbunifu

TAREHE 11 Desemba 2020

ZIFAHAMU MBOLE ZA ASILI NA MATUMIZI YAKE KWA AJILI YA KUOTESHEA MAZAO.



Wapendwa wasomaji wa makala za kilimo katika blog yetu ya Kilimo bora leo tumekuandalia makala nzuri juu ya Mbolea . Mbolea kwa maana ya kueleweka kwa haraka ni kitu chochote kinacho ongeza virutubisho muhimu kwenye udondo ambavyo hutumiwa na mimea ili kuboresha ukuaji wa mimea na upatikanaji wa mavuno mazuri.

Kuna aina mbalimbali za mbolea kama mbolea za asili Mbolea za asili mfano, Samadi, Mboji, mbolea za kijani na Mbolea za viwandani mfano DAP, YaraMila

1. Mbolea za asili

Mbolea aina ya Mboji (Mabaki ya Mazao). Mbolea hizi hutokana na vinyesi vya wanyama, mabaki ya mazao shambani, majivu na takataka nyingine ambazo ni rafiki kwa mazao na udongo (takataka zisizo na madhara kwenye udongo).

Mbolea za asili zinafaa sana kutumika wakati wa kuandaa shamba/ mkulima anaweza kuchamganya mbolea ya asili na udongo wakati wa kulima au mkulima kuitumia mbolea ya asili kupandia mazao yake mfano mahindi, mharagwe, mboga mboga na mazao mengine.

Mbolea za asili hufanya kazi ya kuboresha hali ya udongo kuufanya udongo uwe na uwezo wa kuifadhi maji na hewa, vilevile mbolea za asili ufanya udogo kuweza kutengeneza matundu mazuri ambayo husaidia mizizi ya mazao na hewa kupenya kwa urahisi.

<http://kilimoboratz2.blogspot.com/2017/12/zifahamu-mbole-na-matumizi-yake-kwa.html>

Kilimo ni lazima kuwezesha na kuongeza afya ya udongo, mimea, wanyama na binadamu. Udongo ni nguzo muhimu katika maisha ya viumbe wote kwa ujumla. Udongo ulioharibiwa hauwezi kuzalisha chakula vizuri, na hakutakuwa na malisho ya kutosha kwa ajili ya mifugo.

Ili kuweza kupata chakula cha kutosha kwa ajili ya binadamu na malisho kwa wanyama, ni lazima kuboresha rutuba katika udongo. Afya ya binadamu na wanyama inaunganishwa moja kwa moja kwenye umuhimu na uwezo wa udongo kuzalisha.

Tumia mbolea ya asili kukuzia mimea

Kuna faida nyingi zinazotokana na matumizi ya mbolea za asili kama mboji na nyinginezo. Mbolea asili hutokana na kuoza kwa vitu vyenye uhai kama vile majani, miti na mabaki ya vyakula.

Vitu hivi vinapooza hugeuka na kutengeneza virutubisho ambavyo husaidia kurutubisha udongo na kupunguza gharama kwa mkulima kwa kuwa vitu vinavyotumika ni vya asili. Mbolea ya kukuzia mimea inatokana na tope chujio, au mbolea hai inayotokana na kinyesi cha ng'ombe.

Namna ya kutengeneza

Mbolea hii hutengenezwa kwa kuchanganya kinyesi na kiasi cha maji ili kuweza kunyunyiza kwenye mimea na kutoa matokeo ya haraka kwa muda mfupi.

Mahitaji

Ndoo ya lita 40, kiroba (mfuko), mti, maji, na mbolea hai.

Kutengeneza

- Weka maji robo tatu ya ujazo wa juu kwenye ndoo
- Weka mbolea hai kwenye mfuko ukiwa umeutumbukiza kwenye maji hayo, huku ukiwa umeshikilia kwenye mti uliokatiza juu ya ndoo.
- Funga baada ya maji kujaa kwenye ndoo
- Acha kwa muda wa siku 3, kasha zungusha taratibu ili kukamua
- Rudia zoezi hilo kila baada ya siku 3
- Acha kwa muda wa siku 14, hapo mbolea maji yako itakuwa tayari kwa ajili ya kunyunyizia kwenye mimea yako ili kuikuza

Matumizi

- Tumia gramu 100 kwa kila mche (unaweza kutumia kikopo cha mafuta kupima).
- Unapoweka mara moja, mboga zitastawi vizuri mpaka wakati wa kuvuna bila kurudia tena.

Mbolea hii ya maji inafaa tu endapo unatumia mbolea mboji kwenye shamba lako. Baada ya siku 14 usitumie tena mbolea hii kwani baada ya hapo itabadilika na kuwa dawa badala ya mbolea.

Faida za mbolea za asili

1. Gharama nafuu. Huhitaji kuwa na mtaji mkubwa wa kifedha ili kupata aina hii ya mbolea. Kikubwa zaidi pengine ni gharama za kusafirisha mbolea hiyo.

2. Mbolea ya asili huongeza, kujenga na kukuza mpangilio wa udongo. Hufanya hewa kupenya kwenye mchanga na husaidia utoaji maji shambani hasa kuzuia

mmomonyoko wa udongo. Mbolea hii hufanya mchanga kuwa na maji au unyevunyevu wakati wa Kiangazi. Kwa kutengeneza mpangilio wa mchanga, hufanya mimea kupata rutuba kwa urahisi na kukua kwa afya na kutoa mavuno mengi.

3. Kutunza ubora wa udongo, Mbolea ya asili hutunza ubora wa udongo kwa kuongeza madini yanayohitajika na mimea. Hii inasaidia kuongeza mazao ya mimea.

4. Kupunguza wadudu wa mimea walioko mchangani, hivyo mimea kuwa na nguvu, afya na hustahimili magonjwa na wadudu waharibifu.

5. Haibebwi na mvua au kuhamishwa. Mbolea ya asili haibebwi na maji ya mvua kama ilivyo mbolea za kemikali, hivyo inaifanya kuwa na sifa ya kudumu kwa muda mrefu.

6. Kuondoa wadudu rafiki wa mmea. Hii ni tofauti na mbolea za kemikali ambazo huvutia wadudu waharibifu na kuondoa mazingira rafiki ya wadudu muhimu.

7. Huupatia mmea virutubisho vingi. Mbolea za viwandani zina virutubisho baadhi kwa kiasi fulani zaidi ya vingine. Lakini mbolea za asili zina utajiri wa virutubisho.

8. Huwezesha mizizi ya mmea kukua vizuri kuelekea kwenye virutubisho muhimu. Hii hufanyika kutokana na kuboreshwa kwa muundo wa udongo.

Kama udongo ulikuwa umeshikamana, unapowekewa mbolea asili huwa laini, hivyo kurahisisha mizizi kupenya kwa urahisi.

9.Kuongeza 'ph' ya udongo. Moja ya matatizo yanayopunguza uzalishaji ni mkulima kuwa na udongo wenye ph ya chini dhidi ya mazao yake.

Kwa kuweka mbolea ya asili, ph huongezeka hivyo kuuweka mmea katika hali nzuri ya kuongeza uzalishaji.

Hasara za mbolea ya asili

1.Mbolea ya asili haiwezi kuokoa mmea unaokufa, kwa sababu huchukua muda mrefu kuchukuliwa na mmea. Wakati mbolea ya viwandani ikishaloanishwa tu haraka huchukuliwa na mmea. Mbolea ya asili inahitaji kuoza zaidi na kuvunjwawunjwa.

2.Upatikanaji wake ni mgumu. wakulima wengi wanashindwa kupata mbolea ya asili kwa haraka. Hii ni kutokana na wafugaji wa wanyama kama ngombe kuwapo maeneo ya mbali.

3.Huhitajika kwa wingi. Kwa mfano, kwa ekari moja mkulima anaweza kuhitaji kuanzia tani 12, kwa sababu mbolea asili inahitajika kuwekwa kwa wingi.

Mathalani, katika kila shimo, utapaswa kuweka mbolea inayoweza kujaa viganja vya mikono miwili. Kama ni katika matuta huwekwa kuanzia toroli tatu kwenye tuta la urefu mita 9 na upana mita 5.

4.Huathiri mmea, inaweza kukausha mmea mara moja kama itawekwa bila kuzingatia hali ya mbolea hiyo. Kwa mfano, kama itawekwa ikiwa haijaoza vyema inasababisha mmea kuungua na kukauka.

Lakini pia ikiwekwa ikiwa mbichi inaweza kusababisha mmea kupata magonjwa ya fangasi na bakteria.

5.Ni ngumu kujua virutubisho unavyoongeza. Mbolea za kemikali huwa na virutubisho vikuu vitatu kwa ukuaji bora wa mmea wako.

Hivyo wakati mkulima anaweka, hujua kabisa kiwango anachoweka cha naitrojeni, fosiforasi na potasiamu. Kwa mbolea ya asili, mkulima hawezi kujua ameweka kiasi gani cha virutubisho hivyo muhimu.

Msisitizo

Mbolea ya asili ni njia nzuri mno ya kulisha mimea kuliko kutumia mbolea ya kemikali. Mbolea za kemikali japo hutoa rutuba kwa mimea, hazitengenezi mpangilio au hali ya mchanga.

Ilipakuliwa:28/12/2021

Inapatikana: <https://www.mwananchi.co.tz/mw/habari/makala/mbegu-ya-thahabu/uzuri-na-ubaya-wa-mbolea-za-asili-2831696>

<https://www.facebook.com/mkulimambunifu/posts/mbolea-hai-na-madawa-asili-ni-muhimu-kwa-mimemea-wanyama-na-binadamumkulima-anapo/4797072353667526/>